CHAMA CHA KITUME CHA MTAKATIFU THERESIA WA MTOTO YESU UPENDO GROUP- JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

I. HISTORIA FUPI

Chama hiki kilipokelewa rasmi katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam tarehe 27/09/2020 na Askofu Mkuu Jude Thadaeus Ruwa'ichi OFM CAP, wa Jimbo Kuu la Dar es salaam.

Kabla ya hapo kilikuwa katika ngazi ya Dekania ya Ubungo kikilelewa na aliyekuwa Dekano wa Ubungo Hayati Monsinyori D. Mbiku, ambaye alikuwa pia Paroko wa Parokia ya Chuo Kikuu.

Kilianzia Parokia ya Kimara kati ya mwaka 2008 na 2009, lakini kiliimarika zaidi katika Ngazi ya Dekania kuliko katika ngazi ya Parokia kilikozaliwa.

II. KWA NINI KUITWA "UPENDO GROUP"

Jina hili lilitokana na Kitabu cha Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu **"UA LA UPENDO".**

Licha, ya mambo mengi ya kuvutia yaliyoelezwa katika kitabu hiki, kulikuwa pia na sura zilizoelezea kwa kina Fadhila za Upendo za Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu na jinsi alivyofurahi kuonja Matunda ya Upendo.

Upendo Group ni kikundi au vikundi vya wavulana na wasichana wengi wao wakiwa ni wajasiriamali waliovutiwa na maisha ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu na hivyo kudhamiria kuziiga na kuziishi fadhila zake za Imani na Upendo katika jitihada zao za kumfuata Kristu.

Baada ya kupokelewa Jimboni na katika kikao kimojawapo cha Halmashauri Walei Jimbo Kuu ilipendekezwa jina liboreshwe zaidi ndipo likapatikana jina la "Chama cha Kitume cha Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Cha Wajasiriamali – Upendo Group" cha Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

III. MISINGI MIKUU YA UTUME

(i) Kueneza Upendo wa Mt. Theresia wa Mtoto Yesu katika Jamii kuanzia mtu mmoja mmoja, Familia, Jumuiya, Kanda,

Parokia, Jimbo hadi Kanisa zima na Binadamu wote kwa kuzingatia Urithi bora wa Mila na Desturi za Kiafrika zilizoangazwa na Roho Mtakatifu, Injili, Kitabu cha Katekisimu ya Kanisa Katoliki (The Catechism of the Catholic Church) na mafundisho ya Kanisa Katoliki kuhusu Jamii (The social Doctrine of the Church).

(ii) Kujenga mahusiano mazuri baina ya waamini na waamini, viongozi na waamini, viongozi kwa viongozi wenye nia ya lengo la kuimarisha na kueneza Upendo miongoni mwao.

(iii) Kupenyeza Injili katika biashara ikizingatiwa kuwa kipaji cha biashara ni moja wapo ya karama za Roho Mtakatifu na kwamba kipaji hicho kitumike katika shughuli zote za biashara kwa lengo la kukuza Utu, Haki, Upendo na Maendeleo ya binadamu kimwili na Kiroho kwa sifa na utukufu wa Mungu.

IV. CHIMBUKO LA UTUME

(a) Tukio lililoshuhudiwa na mwandishi wa nakala hii mbele ya FR. VICMISSIEN (M.A) na SR. JANE (MSOLA) katika eneo la Kimara Baruti – Wilayani Ubungo mfanya biashara mmoja wa magrili na papo hapo fundi wa kutengeneza magrili hayo alimfukuza kwa upanga wenye ncha kali Mhubiri mmoja wa Kilokole aliyeshika Biblia katika mkono mmoja na mkono mwingine ukitafuta aya alizofikiria zilifaa amsomee yule mfanya biashara wakati akiwa “Busy” na utengenezaji wa bidhaa zake. Wote watatu walishikwa na butwaa kwa tukio hilo. Swala lilikuwa ni kwanini mtu aliyefika na Neno la Mungu, Neno la Uwokovu kwa mfanya biashara afukuzwe kana kwamba angekuwa ni mwizi au jambazi mkubwa. Baada ya kuvaa ujasiri na kumhoji yule mfanyabiashara ni kwa nini alimfukuza kama mbwa yule Mtumishi wa Mungu aliyemletea neno la Uwokovu na neno la Amani?

Jibu lake lilikuwa, ili afanikiwe katika biashara yake na kupata faida ilibidi kutumia mbinu ya udanganyifu katika kupanga bei na kadhalika.

Neno la Mungu – Biblia inataka ukweli na Uaminifu. Fadhila hizo kwake yeye alisema ni kikwazo kikubwa katika kupata faida na hivyo Biblia haitakiwi kamwe katika sehemu zake za kazi. Amsubiri mpaka Jumapili atakapokuwa Kanisani amletee mahubiri yake, naye Atamsikiliza. Alisisitiza.

(b) Mtazamo wa mwandishi wa Makala hii, hapo aligundua kulikuwa na dalili za mpasuko katika uelewa wa watu juu ya uhusiano kati ya Enjili na Biashara. Yule fundi wa magrili aliwawakilisha watu wote wanaodhania kuna mgongano (conflict) kati ya Engili na Biashara. Baada ya kufanya utafiti wa kina mwandishi wa Makala alifikia kugundua kuwa wengi wanaendeleza uwepo wa mgawanyiko kati ya Enjili na Biashara. Kwa maslahi ya kibiashara watategemea nguvu za giza na Imani za Kishirikiana. Kwa maslahi ya Engili watamtegemea Mungu. Hapo ilikuwa Dhahiri ni muhimu kuanzisha Utume utakaokuwa na Jukumu la kubomoa ukuta uliopo kati ya Enjili na Biashara.

Fr. Vic Missien (M.A) licha ya kutangulizana na Sr. Jane (Msola) alikuwepo pia Sr. Sophy (Msola) ambaye alikuwa amebakia nyumbani na hakuwa katika eneo la tukio. Huyo aliiachia familia na Jumuiya ya mwandishi wa Makala hii utaalamu na Ujuzi kutengeneza Sabuni za miche, divai kutoka maindi makavu, Jam kutoka Maganda ya maembe au machugwa n.k. Familia hiyo ilizingatia zaidi utaalamu wa kutengeneza Sabuni za miche na **ndio uliotumika kuanzisha kikundi cha kwanza cha wajasiriamali ambacho kiliitwa "UPENDO SABUNI" NDICHO** KILIKUWA KIKUNDI CHA KWANZA CHA UPENDO GROUP na wanachama wake wakwanza walikuwa ni:-

1. **Bertha Mroso**
2. **Juliana Msofe**
3. **Germana Nyoni**

Na walezi wa kwanza wa kikundi hicho ni:-

1. **Mapadre wa Shirika la Mt. Claret Mfn. Fr. Francis CMF na waliomfuata akijumuishwa Fr. Timothy CMF.**
2. **Masista wa Shirika la Mt. Theresia wa Mtoto Yesu Mfn. Sr. Mamertha, Sr. Elvila, Sr. Clara Sr. Matrona na wenzake.**
3. **Mabinti wa Mt. Paulo Dar es salaam Sr. Mary, Sr. Theresia na wengine wote**
4. **Marehemu Maud Jackson**
5. **Marehemu Anna Salema**
6. **Marehemu Anna Temu**
7. **Mr. Santori Sande**
8. **Silverius C. Komba**
9. **Christopher Mpangala**

Mwandishi wa Makala hii alipendekeza kikundi hicho kiandaliwe kuwa Chama Cha Kitume na Utume wao uwe ni wa kupenyeza

Enjili katika Biashara. Na Mlezi wa Kikundi hiki alipendekezwa awe ni Mt. Theresia wa Mtoto Yesu kutokana na fadhila zake za Upendo, Unyofu wa Moyo, Imani thabiti n.k zinge kuwa nyenzo bora katika kufanikisha Utume wa kupenyeza Enjili katika Biashara.

Fr. Francis CMF Paroko wa wakati ule alilipokea wazo na kulibariki, na alilipeleka kwa Askofu Mkuu wa wakati ule Kadinali Pengo, alilipokea na kulibariki.

Ndipo Katiba ya awali ya Upendo Group iliandaliwa na kupitishwa na Monsinyori D. Mbiku katika ngazi ya Dekania ikatumika mpaka tarehe 27/09/2020 ndipo ilipoanza kutumika Katiba mpya ya Jimbo Kuu chini ya Mlezi mpya ambaye ni Fr. Patrick Musumba CMM ambaye bado anaendelea.

V. UANACHAMA

(a) Kuna aina tatu za uanachama
Kama ifuatavyo: -
- (i) Uanachama wa wwanzilishi
- (ii) Uanachama wa kawaida
- (iii) Uanachama wa waheshima

(b) Utaratibu wa kuingia
- (i) Mtu mmoja mmoja anaweza kujiunga na kikundi au Taasisi iliyopo kwa kufuata masharti yaliyoainishwa
- (ii) Kikundi hasa chenye wazo la biashara Halili Fulani kinaweza kujiunga na chama kitapewa jina kulingana na aina ya biashara kinachofanya au kunachotarajia kufanya ili mradi idadi ya chini kabisa ya kuanzia ni watu watatu.
- (iii) Sifa za mwanachama
  - (a) Awe Mkatoliki mwenye umri wa miaka 18 au zidi, awe na akili timamu.
  - (b) Asiwe na kizuizi cha kupata Sakramenti
  - (c) Awe na Imani katika misingi Adili ya mafundisho ya Mtakatifu Theresia wa Mtoto yesu. Apende kuongozwa na Fadhili kuu za Mt. Theresia wa Mtoto Yesu katika maisha yake ya kila siku, ndni ya familia, jamii na katika biashara zake ambazo ni Upendo, Unyenyekevu na Unyofu wa Moyo.
  - (d) Awe na mahusiano mazuri ya kushirikiana na kushirikishana na wenzake katika shughuli za chama/kikundi

(e) Awe na uwezo wa kuwa na kikundi chenye wazo la biadhara.
(f) Awe tayari kutii uongozi wa Kanisa na ngazi za Kisheria.
(g) Ashiriki Semina za Kiroho Pamoja na kuabudu Ekaristi Takatifu.
(h) Awe na dhamira na wazo la kuzingatia Injili katika biashara, ili mradi shughuli za kibiashara ziangazwe na ziongozwe na ujumbe wa Injili Takatifu na zielekeze mshiriki kwenye Wokovu.
(i) Kama mwanachama ni kikundi basi wanacham katika kikundi hicho wawe na sifa (a) hadi (b) katika kanuni hii.
(j) Azikubali/kuikubali na awe/kiwe tayari kuzifuata kikamilifu kanuni hizi.

VI. MASHARTI YA UTARATIBU WA KUWA MWANACHAMA

(a) Mwanachama mwanzilishi: -

Atakuwa mwanachama kwa kuwa kwake kati ya waanzilishi ambaoni wale watakao kuwa wanachama hai wa moja wapo wa vikundi vinavyotaja katika kanuni (iii).

(b) Mwanachama wa kawaida: -

Mtu atakayetaka au kikundi kinachotaka kuwa mwanachama wa kawaida atafuata/kitafuata utaratibu ufuatao:-

(i) Ataandika/kitaandika barua ya maombi kwa katibu.
(ii) Kamati itayajadili maombi yao na ikiridhika na sifa za mwombaji itamkubali/itakikubali kwa maandishi kuwa mwanachama/wanachama kwa masharti yaliyowekwa na au yatakayowekwa kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizi.

(c) Mwanachama wa Heshima

Sifa ya kuonyesha Moyo wa kukisaidia chama au kikundi husika kwa hali na mali.

(d) Haki za mwanachama na wajibu wake

(i) Kuwa mwanachama mwanzilishi na wa kawaida.

- Kuhudhuria na kutoa Mawazo katika vikao au mikutano inayomhusu.
- Kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi.

- Kupelekewa taarifa za mikutano katika muda muafaka ukiwa sio chini ya siku tatu kabla ya mkutano husika.
- Kuinjilisha kupitia biashara.
- Kuhudhuria semina za ujasiriamali
- Kujitolea kwa hali na mali, kwa ajili ya kikundi chake kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa au zitakazowekwa mara kwa mara kwa kuzingatia kanuni hizi.
- Kulipwa mgao wake au kupewa riziki yake kwa mujibu wa kanuni hizi na masharti na taratibu rasmi na muafaka wa chama au kikundi chake zilizowekwa au zitakazowekwa mara kwa mara kwa zingatia kanuni hizi.

(ii) Na wajibu wake: -

- Kuwa muadilifu na kujitoa kwa ajili ya kutimiza madhumuni, mipango, na malengo ya kikundi husika.
- Kuhudhuria mikutano inayomuhusu
- Kulipa kiingilio na ada yam waka kama ilivyopangwa na kamati.
- Kuhudhuria semina za ujasiriamali.
- Kuchagua na kukubali kuchaguliwa kuwa kiongozi.
- Kuinjilisha kupitia biashara.

(iii) Mwanachama wa heshima

Haki za mwanachama wa heshima

- Kuhudhuria na kutoa Mawazo katika vikao na mikutano atakayo alikwa.
- Kushauri pale panapostahili
- Hatakuwa na haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi.
- Hatatakiwa kutoa kiingilio bali kwa hiari yake ataweza kutoa michango yoyote na kwa kiwango chochote kwa ajili ya kikundi au chama.
- Hatakuwa na haki ya kupiga kura au kulipwa chochote akiacha au kusitishwa uanachama wake wa heshima.
- Hatakuwa na haki ya kupokea mgawo au riziki yoyote kwa mujibu wa kanuni hizi.

VII. KUACHA AU KUSITISHWA UANACHAMA

Uanachama wa mwanachama utakoma au kusitishwa ikiwa:-

(a) Amefariki dunia.
(b) Amevunja masharti/kanuni
(c) Ana ugonjwa wa akili
(d) Amefungwa kwa kosa la jinai
(e) Amejiuzuli kwa maandishi
(f) Amehama au amehamishwa kutoka eneo la chama chake.

VIII. TAASISI ZA UPENDO GROUP:

Ili kuweza kufikia lengo kuu la Upendo Group kuleta uwokovu wa Kiroho na kimwili kwa wajasiriamali Upendo Group imelazimika kuanzisha Taasisi kadhaa za kutekeleza lengo hili kuu kwa vitendo.

Taasisi zote zinaunganishwa na Utume mmoja wa Upendo Group wa kupenyeza Enjili katika biashara au K;uinjilisha biashara. Walengwa wakuu ni wajasiriamali wadogo wadogo ili waweze kuinuliwa kiuchumi na Kiroho kutoka point A mpaka point B na kuendelea.

Taasisi zote lazima zizingatie misingi iliyoainishwa awali ya Utume wa Upendo Group katika Utendaji wao.

TAASISI HIZO NI HIZI HAPA: -

(1) **WAJASIRIAMALI WADOGO WADOGO**.

Vikundi vya wajasiriamali katika maeneo tofauti tofauti huundwa katika maparokia. Huanzisha vikundi kwa mfano wa watengeneza Divai, au Sabuni, au Batiki n.k. hujigawa katika vikundi vya watu watatu watatu au zaidi. Kila kikundi huwa na mwenyekiti, katibu na mhazini. Uongozi katika ngazi ya vikundi hushughulikia biashara, wanachozalisha ni chao na hutumika kwa mahitaji ya familia zao, kulipia elimu, matibabu malazi, mavazi n.k kila kikundi kinakuwa huru na kinatunza siri zake.

Vikundi kadhaa katika Parokia hiyo huunda mfuko wa Pamoja ambao kila kikundi huchangia kadri ya uwezo. Mfuko huu ni mali ya Parokia na chochote kilichokusanywa hupelekwa kwa Baba Paroko ili aweze kukitumia kadiri atakavyoona inafaa kwa maendeleo ya Parokia yake. Mhazini kutoka Kamati Tendaji ya Upendo Group ngazi ya Parokia ndio kiungo muhimu kati ya Paroko na mfuko huu.

Vikundi kadhaa ndani ya Parokia hujumuika na kuchagua Kamati Tendaji ngazi ya Parokia. Kimsingi kila kikundi pale vikundi vinapokuwa vitano au pungufu kinatakiwa kuwa na mwakilishi mmoja katika Kamati Tendaji ya Parokia. Uchaguzi katika ngazi hii huzingatia Katiba ya Halmashauri Walei Taifa. Uchaguzi katika ngazi ya vikundi hizingatia Katiba ya Upendo Group.

Kazi kubwa ya Kamati Tendaji ngazi ya Parokia ni kusimamia maswala ya Uenjilishaji kwa mfano semina za Kiroho, Matendo ya Huruma, Hija Pugu/Bagamoyo za Kijimbo na za Kiparokia n.k. na kusimamia maswala ya Amani kwa vikundi vyote vya Upendo Group katika Parokia husika

Kazi kubwa ya viongozi ndani ya vikundi ni kusimamia maswala ya biashara ya vikundi hivyo kama vile maswala ya uzalishaji, masoko, project write – ups uchangiaji katika mfuko wa Pamoja ambao kimsingi ni mali ya Paroko Pamoja na Semina za Ujasiriamali.

(2) UPENDO SACCOS: -

Hii inafahamika zaidi na makao makuu yake yako katika Parokia ya Maria Magdalena Kimara Mtoni.

Riba ya mikopo yao iko chini sana percent 1 – 1.4% ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo kupata mikopo kwa riba nafuu kutoka Upendo Saccos.

(3) UPENDO NGO (UPENDO CATHOLIC EMPOWERMENT INITIATIVE(UCEI)

Hii inalenga kuwasaidia wajasiriamali na watu wengine wote katika maeneo matatu ambayo ni:-

(i) Ujasiriamali/biashara
(ii) Afya na
(iii) Elimu

Taasisi hii ina mwaka mmoja tangu ianzishwe. Ilizinduliwa na Mhashamu Askofu Stefano Musomb awa Jimbo Katoliki Bagamoyo. Ilizinduliwa alipokuwa bado Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es salaam. Katika Parokia ya Mt. Perto (Osterbay) kwa niaba ya Askofu Mkuu Jude Thaddaeu OFM CAP wa Jimbo Kuu la Dar Es Salaa.

Makao makuu ya NGO hiyo na ofisi yake iko katika Parokia ya Mt. Perto.

(4) MFUKO WA UPENDO MSAMARIA MWEMA

Taasisi hii ilipokelewa na Mhashamu Askofu Mkuu lakini bado kusajiliwa serikalini mpaka hapo Mhashamu Askofu Mkuu atakaporidhia isajiliwe. Mfuko huu ulilenga kutatua au kupunguza changamoto za wana Upendo Group na za waamini wote wa Jimbo Kuu wanaokabiliwa na changamoto za misiba au Mikasa mbalimbali na zinahitaji majibu ya papo kwa hapo.

Tuseme Taasisi hii bado kuanza rasmi mpaka hapo Mhashamu Askofu Mkuu atakaporidhia mfuko uanze.

(5) TAASISI YA GAZETI LA UPENDO DAIMA MTANDAONI.

Ni gazeti la mtandaoni la Jimbo Kuu la Dar es salaam litasaidia sana kuinua biashara za wajasiriamali kwa kuwaunganisha na masoko husika na pia litainua sana Utume wa Upendo Group wa kupenyeza Enjili katika biashara. Gazeti hili liko Jirani kuanza Ofisi za gazeti ziko katika Jengo la Atiman House kwa hisani ya Mapadre wa Shirika la Wamisionari wa Afrika.

Gazeti pia litasaidia kuinua magazeti ya Tumaini letu na Kiongozi kwa kuwaalika na kuwapa fursa ya kutumia “Portal” ya Upendo Daima mtandaoni ili waweze kuwafikia watu wengi zaidi.

(6) KWAYA YA MT. THERESIA WA MTOTO YESU YA UPENDO GROUP.

Ilianzishwa kwa madhumuni makuu mawili:-

(1) Kuwa ni kumbukumbu hai nay a kudumu ya miaka 25 ya Uaskofu wa Mhashamu Askofu Mkuu Jude Thaddaeus Ruwa’ichi OFM CAP.

(2) Chombo cha kueneza Utume wa Upendo Group na kupenyeza Enjili katika biashara n awa kutangaza misingi ya Utume wa Upendo Group kupitia nyimbo mbalimbali zitakazotungwa.

(3) Ni Chombo cha kuwaunganisha wana Upendo Group Jimboni Dar es Salaam. Hufanya mazoezi yao kila Jumapili kuanzia

saa 10 jioni katika Parokia ya Magomeni. Na makao makuu ya kwaya hii yako katika Parokia ya Familia Takatifu Mbura Hati. Inalelewa na Viongozi wetu wawili ambao ni:-

(i) Fr V. Kasembo Mkurugenzi Tume ya Walei Jimboni na Paroko wa Parokia ya Familia Takatifu Mburahati
(ii) Fr. Partick C. Musumba CMM. Mlezi wa Upendo Group Jimbo kuu la Dar es salaam na Mwakilishi wa Askofu Mkuu katika Utume wa Upendo Group.

Kwaya hii huongozwa pia na Katiba ya UKWAKATA na hufanya shughuli zake kwa kushikiana na UKWAKATA. Yeyote anayejisikia kupenda kumtukuza Mungu, kupita kwaya hii anakaribishwa wasiliana na Baba Mkurugenzi au Baba Mlezi na au Maria Mathiasi, Mwenyekiti wa hii kwaya kwa simu na 0656 091 107.

Mipango inafanyika ya kuiruhusu kwaya hii kupita kuinjilisha katika Parokia mbalimbali ndani ya Jimbo Kuu la Dar es salaam.

IX. MATARAJIO YA BAADAYE

(i) Kueneza Utume wa Upendo Group katika Majimbo yaliyoko chini ya Jimbo Kuu la Dar es salaam na Majimbo mengine pia.
(ii) Kuanzisha Taasisi zaidi.
  (a) Redio ya Upendo Daima Mtandaoni
  (b) Tv ya Upendo Daima Mtandaoni
  (c) Chuo Kikuu cha Mt. Theresia wa Mtoto Yesu cha Mtandaoni ndani ya Jimbo Kuu la Dar es salaam.

X. VIONGOZI WA UPENDO GROUP – JIMBO KUU

MWENYEKITI:
SILVERIUS COSMAS KOMBA
SIMU: 0756 601 115

MAKAMU MWENYEKITI
ANNA BASITA
SIMU: 0658 278 691

KATIBU
EDWIN CHAPA
SIMU: 0656 652 250

KATIBU MSAIDIZI
EPHREM MKENDA
SIMU: 0713 216 677

MHAZINI
ANNA MWIKOMBE
SIMU: 0713 249858

MHAZINI MSAIDIZI
ANNANIAS RUTAMBUKA
SIMU: 0754 750 113

BABA MLEZI: PADRE PATRICK MUSUMBA CMM
MWAKILISHI WA ASKOFU MKUU KWA UPENDO GROUP
NA TAASISI ZAKE ZOTE

MWENYEKITI WA BODI YA GAZETI: FR.C. NGOWI OFM CAP.

MWENYEKITE WA BODI YA SACCOS: DR A. MERU

MWENYEKITI WA BODI YA UCEI (NGO): DR J. KAKENENO

MLEZI WA KWAYA: FR. V. KASEMBO
MKURUGENZI TUME WALEI